**Kila mtu ana malaika (09) - Maambukizi ya ukimwi kutoka kwa mama hadi kwa mtoto**

Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

**Wahusika:**

Annie
Jet
Mjomba Imrat
Djamila
Tom
Wavulana

## Utangulizi

Karibu tena katika kipindi cha Sikiliza Ujifunze, ambapo utasikia mchezo wa kuigiza Kila mtu ni malaika, mchezo unaofuatilia maisha ya vijana wanne na jinsi wanavyokabiliana na matatizo yao ya kimaisha katika mahusiano yao.

Utakumbuka kwamba sasa Angela anaishi na Pinto na hivi karibuni anatazamia kujifungua.Baada ya kugundua ameambukizwa virusi vya HIV sasa anapokea ushauri nasaha na kupata maelezo zaidi kuhusu njia za kuzuia maambukizi ya virusi kutoka kwa mama hadi kwa mtoto yaani PMTCT. Na pia ameshajifunza jinsi ya kuzuia maambukizi ya virusi kwa mtoto wakati wa kujifungua. Kwa upande mwingine rafikiye Annie ameshang’amua kwamba anajihatarisha sana katika maisha yake. Lakini kuuvunja uhusiano wake na baba sukari sio rahisi na bado kasheshe inamsubiri. Djamila nae pia yuko kwenye matatizo. Lakini kwa nini anakwaruzana na mjombawe? Ungana nasi katika sehemu hii ya tisa ya mchezo "Malaika wa kila mtu"

## Tukio la Kwanza: Ndani ya Nyumba

| | |
|---|---|
| SFX | Ngurumo za radi zinasikika kwa mbali kutoka nje. |
| ANNIE | Jet, tafadhali unaweza kuiweka chini hiyo karatasi tuzungumze? |
| SFX | Afungua karatasi za gazeti |
| JET | (Atafshika) Hmmmm? |
| ANNIE | (Kwa Upole) Sikiliza! Na tafadhali usikasirike. Mimi sitaki kuja tena hapa kwako. |
| SFX | Afunga gazeti na kuliweka kwa hasira mezani |
| JET | Nini? Wasemaje, Annie? |
| ANNIE | (Kwa sauti ya juu) Nasema sitaki kuja tena kwako umesikia. |
| JET | Oh! Haya ni mapya! Nini kimesababisha haya yote, eh? |

| | |
|---|---|
| ANNIE | Nilikuona kliniki. |
| JET | Uh? Wazungumza kuhusu nini, mbona sikuelewi? |
| ANNIE | Sikiza Jet, nilikuwa kliniki, na nilikuwa nimekwenda kudunga sindano ya kuzuia mimba, nikakuona. Nilifikiri unakwenda kwa mganga tu, nini kilichokufanya kwenda kliniki? |
| JET | (Kwa vitisho) Wanichunguza, nakuuliza sasa: Umeanza kunichunguza? - Enh Kitu gani? |
| ANNIE | Si hivyo Jet, kwa nini hatuwezi kuzungumza kama watu wa kawaida tu? |
| JET | Hmmm. Angalia, hakuna kilichotokea sawa. Dawa za yule mganga hazikufanya kazi, kwa hiyo akanituma kwenda kliniki. |
| SFX | NGURUMO ZA RADI ZASIKIKA KWA SAUTI KUBWA |
| ANNIE | Na daktari kakwambia nini? |
| JET | Funga mdogo Annie, umesikia? Wewe nani kwani? Wewe sio mamangu. |
| ANNIE | Sawa. Ikiwa hatuwezi kuzungumza juu ya maisha yako basi tuzungumze kuhusu mimi. Nafikiri nacheza mchezo wa paka na panya katika maisha yangu. |
| JET | Unaamanisha nini? |
| ANNIE | Maradhi ya kuambukiza ya zinaa kwa mfano. Sote hatutumii mpira wa condom, sawa bwana. Kwa maana hiyo unaweza ukaniambukiza maradhi ulonayo ya zinaa. |
| JET | Mimi? Nimekuambukiza? Na kwa nini niwe ni mimi nimekuambukiza enh? Inawezekana wewe umeniambukiza. |
| ANNIE | Na inakuaje sina maradhi hayo? |
| JET | Ahh sawa basi, hata mimi sina, niko sawa. |
| ANNIE | Na uchunguzi wa damu yako? |
| JET | Sikiza bwana Annie, umenichosha na maswali yako, nimechoshwa na mjadala huu. |
| ANNIE | Lazima uwe umepewa majibu ya uchunguzi wa damu ulofanyiwa kuhusu maambukizi ya maradhi ya zinaa. |
| JET | Hiyo sio kazi yako na haikuhusu,lakini ikiwa ni lazima ujue, basi nilikataa kuchukua matokeo ya uchunguzi wa HIV nilofanyiwa. Na ukiwa huyataki matokeo basi huambiwi majibu na hulazimishwi. |
| ANNIE | Yaani umekataa kujua hali yako? Hilo ndo ninalozungumzia. Maamuzi yako yananiathiri. Angela amegundua kwamba ana… (anyamaza ghafla) aa…aligundua ni mjamzito. |

**Kila mtu ana malaika (09) - Maambukizi ya ukimwi kutoka kwa mama hadi kwa mtoto**

Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

| | |
|---|---|
| JET | Angalia, nesi amenipa mfuko mzima wa condom, sawa? Ikiwa huo ndo wasiwasi wako. |
| ANNIE | Tunachokizungumzia hapa ni juu ya HIV, Jet. |
| JET | Hapana, mimi sina virusi vya HIV. Nina maradhi mengine tu ya zinaa, ntapona tu, na nikimaliza matibabu, hakuna haja ya kutumia mpira wa condom. Una shida na hilo? |
| ANNIE | Ndio ninayo, tena kubwa. Je, ikiwa una virusi? |
| JET | Ikiwa, ikiwa, ikiwa nini wewe? Kila mara lazima useme ikiwa. Sikiza, huu upuuzi juu ya HIV uko tu kututia wasiwasi sisi, sote tutakufa tu siku moja, hakuna atakayebaki. Mimi nalipa karo yako ya shule, lazima ulipe. |
| ANNIE | Jet wewe ni mzee sana kunizidi. Siwezi Kuendelea kuhatarisha maisha yangu wakati una wapenzi wengine chungu nzima. |
| JET | (Kwa sauti ya juu) Na wewe hujui lo lote enhe? |
| ANNIE | Sijasema hivyo. Ninachosema mimi sote wawili lazima tukapime na tutumie mpira wa condom. |
| JET | Una wasiwasi utapata mimba au nini? Unatumia vidonge vya kuzuia mimba. (Ambembeleza) Annie kwa nini huniamini, tafadhali niamini mpenzi. |
| ANNIE | Imeandikwa wazi hapa kwenye mfuko kwamba vidonge vya kuzuia mimba havikuzuii usipate virusi vya HIV na ukimwi. Ila condom tu. |
| JET | Hebu koma kuzungumzia ukimwi na virusi vya HIV kama ambaye umesikia nimeambukizwa. Kama unataka kutumia condom, nenda ukatafute wanaume wengine. Mimi ni mwanamme wa hakika, sio mchezo. |
| ANNIE | Wanaume wa kweli wanawajali wapenzi wao. Ikiwa hutaki kutumia condom basi uhusiano wetu uishie hapa. |
| SFX | MUZIKI WA KUSHTUA CHINI YA SAUTI |
| JET | (Anakasirika) Haya kafie mbele huko, nenda zako. Ukajisimamie mwenyewe. Nenda mtumba wewe Umeshaishiwa Annie. Nenda, chukua begi lako hili hapa, vitabu vyako, toka! |
| SFX | MLANGO WAFUNGUKA, SAUTI YA NGURUMO ZA RADI. |
| ANNIE | Usinisukume, achana na mimi. Waniumiza, Jet. |
| JET | (Anampiga akihema kwa sauti) Nje, toka nje. Huna shukurani, msichana wewe. Nenda. |
| SFX | MVUA KUBWA YANYESHA NA RADI |

**Kila mtu ana malaika (09) - Maambukizi ya ukimwi kutoka kwa mama hadi kwa mtoto**
Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

SFX KISHINDO CHA MTU ANAANGUKA
SFX MLANGO WAFUNGWA
ANNIE (Kwa sauti ya chini) Ooooh. Mguu wangu, jamani nafa! Mguu wangu, ouuuw!
SFX Muziki unafifia.

**SURA YA PILI: NDANI, SAUTI ZA USIKU**

SFX NGURUMO ZA RADI BADO ZINASIKIKA
MJOMBA IMRAT (Anahema kwa sauti ya juu) Djamila usjiweke kando kila mara. Mimi ni mjomba wako. Njoo, njoo karibu, hii itakuwa siri yetu wawili tu.
DJAMILA (Afurukuta) Mjomba Imrat, niache tafadhali.
MJOMBA IMRAT (Anamng'ang'ania huku akihema)
DJAMILA (Apiga kelele) Niache wewe mnyama mkubwa!
MJOMBA IMRAT Huna adabu kabisa, unawezaje kunizungumzia hivyo, huna heshima hata kidogo na wanaume?
DJAMILA Je, heshima yangu? Niondokee.
IMRAT (Ambembeleza) Acha uoga Djamila, nikumbatie tu. Kuna ubaya gani ukinikumbatia? (Kwa ukali) Acha kupiga kelele, mpumbavu.
DJAMILA (Analia) Mjomba, tafadhali mjomba niache. Ntakusema ntamwambia mama, lazima ukome tabia hii.
IMRAT Kwa nini uko hivi, Djamila - umeshakomaa wewe. Unafanya mambo ya utoto kwa nini. Ouch. Agggh! Kaning'ata mpumbavu, zimwi mdogo. Arrgh!
SFX SAUTI ANAKIMBIA AKITEREMKA CHINI
SFX MLANGO WAFUNGUKA NA KUJIFUNGA
SFX MUZIKI KUMALIZIA

**SURA YA TATU: MVUA INANYESHA**

SFX NGURUMO ZA RADI. NDANI YA MKAHAWA, KELELE ZA WATU, MUZIKI
MVULANA WA 1 Vipi Tom - Umelenga vizuri! (Kimya) Tazama, sio Annie yule. Anayechungulia dirishani? Anakuita?
TOM Uh? Oh, ndo yeye. Dez njoo bwana, endelea hapa na mchezo. Ntarudi sasa hivi.
SFX ANAFUNGUA MLANGO
SFX BARABARANI NA NGURUMO
SFX SAUTI ZA KELELE ZA MKAHAWANI ZINASIKIKA CHINI CHINI

**Kila mtu ana malaika (09) - Maambukizi ya ukimwi kutoka kwa mama hadi kwa mtoto**

Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

| | |
|---|---|
| ANNIE | Nimemeukomesha uhusiano Tom! Jet alinifurusha nyumbani kwake bila huruma. |
| TOM | (Kwa hasira) Amekuumiza pia sio? Ngoja niwaite vijana, tutamkorofisha mzee yule, mbwa kasoro mkia! Anawezaje kukupiga. |
| ANNIE | Hapana, hapana Tom, msifanye hivyo, kwanza nashukuru amefanya hivyo, kwa sababu amenizibua masikio, nimemjua ni mtu wa aina gani, sina haja nae. |
| TOM | (Kwa upole) Njoo, ingia ndani ujisafishe. Unaweza kuingia chooni huko kwa wanawake, ukiisha nikuletee kinywaji, sawa. |
| SFX | MLANGO WAFUNGULIWA. KELELE ZA MKAHAWANI. NGURUMO ZA RADI ZAFIFIA. |
| SFX | SAUTI YA BIA INAFUNGULIWA |
| MVULANA 2 | Vipi Tom, mshikaji wangu, chukua basi bia yako nilokuahidi, heko bwana. |
| TOM | Sivyo unavyodhania Moron. Hebu tupeni nafasi, tuzungumze kwenye ile kona pale peke yetu, sawa washikaji? |
| MVULANA 1 | Sawa, hakuna noma, lazima tuwasaidie dada zetu bwana, au sio? |
| SFX | KELELE ZA VIJANA/WAKIGONGEANA MIKONI NA VICHEKO |
| TOM | (Kando ya Mic) Niko hapa, Annie. (Kwenye Mic) Kinywaji chako hiki. |
| ANNIE | Asante. (Anakunywa kidogo) Tom, nataka kuanza upya maisha yangu. Huu ndo mwaka wangu wa mwisho shule. Nahitaji kuwa na mtazamo na kuachana na tabia ya kuhatarisha maisha yangu. |
| TOM | Waonekana kama hatimae umegutuka kutoka usingizini! |
| ANNIE | Unajua Tom, ulinambia kweli wakati ule ulinambia huna haja na mimi kwa sababu sijitambui kwa kulala lala ovyo na wanaume bila ya condom. |
| TOM | Samahani sana, nilitumia maneno mazito sana. |
| ANNIE | Ndio yalikuwa mazito, lakini yamesaidia. |
| TOM | Basi mimi nilidhani ulitaka kujaribu kujiua, enh, unaishi katika hatari na kwa nini lakini Annie? Kwa mtu mzima kama yule na yule dereva wa taxi aliyeweka akili zake kwenye chupi! Aah Annie. |
| ANNIE | (Kicheko, halafu kimya) Tom, unaujua umasikini wewe? Yaani namaanisha ule ufukara kabisa umeshawahi kuushuhudia? Yaani nyumbani hamna chakula. |

| | |
|---|---|
| | Babako hayuko, mama anahangaika peke yake kukutafutia, we acha tu. |
| TOM | Hapana Annie, sio kweli. |
| ANNIE | Tom, hali hiyo ilinifanya mimi nikaanza maisha haya nilianza na kupokea vijizawadi vidogo vidogo kutoka kwa wavulana, peremende, chips, juice, halafu nikipata zawadi hizo nakubali kuwapiga mabusu, kuwakumbatia, halafu mambo yakazidi. Mimi ni mtoto wa pekee katika familia ambayo haikuwa na baba, na mamangu hana kazi. Nilitaka kupendwa na hivi vijizawadi vilisaidia sana kutunasua kutoka kwenye ufukara. Jet alitupa televisheni na mamangu anatazama vipindi vya TV bila ya kupumzika. Lakini muhimu zaidi kwangu ilikuwa karo ya shule. |
| TOM | Lakini wasichana wengi hawajiingizi katika tabia hii, eti kwa sababu ya umaskini, wanataka tu kupata mavazi ya fesheni za kileo, simu na mambo mengine ya anasa. |
| ANNIE | Ni kweli Tom, na hilo ndo lililonikutana. Maanake sasa iligeuka na kuwa tabia yangu, ikawa ni mazoea. Sihitaji kujiuza mwili wangu kiasi hiki na naogopa. (Apumua kwa sauti) Nataka kujifahamu, kujijua Tom! |
| TOM | (Aelewa) Ahh! Unataka kupima. Nakwambia Annie, ukipima utafanya jambo zuri sana,utajihisi mwenye nguvu na utakuwa ukiyaendesha maslahi yako binafsi. (Kimya) Nikusaidie vipi? Twende pamoja? |
| ANNIE | Utakubali Tom? Nitafurahi sana, nilitaka kumwambia Angela anipeleke lakini anakaribia siku zake za kujifungua. |
| TOM | Wow! Inashangaza. Kwa hivyo ikiwa tutakwenda kliniki basi nachagua twende ya mjini au… |
| ANNIE | (Anapumua) Naelewa! Ili watu wasitutambue! |
| TOM | Sio hivyo aah Annie,kwa kweli nilitaka kusema, unajua nesi wa kliniki ile ni mrembo zaidi kuliko wa kliniki ya Matula! |
| ANNIE | (Kicheko) Anha Tom! Asante sana! |
| TOM | Kwa nini? |
| ANNIE | Kwa kunifanya nicheke namna hiyo! |
| SFX | Muziki wa kumalizia. |

**Hitimisho**

**Kila mtu ana malaika (09) - Maambukizi ya ukimwi kutoka kwa mama hadi kwa mtoto**

Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

"Kila mtu ni malaika" ni mchezo wa kuigiza uliotungwa na Romie Singh na kuhaririwa na Saumu Mwasimba. Hadi hapo ndio tumefikia mwisho kwa leo katika kipindi cha sikiliza Ujifunze. Jiunge nasi tena katika sehemu ya kumi na ya mwisho ya mchezo huo.Angela anajaribu kumshawishi Pinto kwamba wanaweza kupanga maisha yao ya baadae ikiwa wataijua hali yao ya afya kuhusu virusi vya HIV na kupata matibabu yanayohitajika. Angela anakutana na marafiki zake wa zamani Djamila na Annie ambapo pia wamekuwa wakijifunza kuishi na hatari pamoja na mabadiliko yanayojiri kwenye maisha yao.

Kumbuka unaweza kuusikiliza tena mchezo huu au kuwaambia marafiki zako juu ya mchezo huo kwa kutembelea tovuti yetu, anuani yetu ni www.dw-world.de/lbe.

Kwa heri.